

Pambazuko Ukweli Hauna Kutu

Toleo Namba 00001

Jumatatu-Julai 11, 2022

Tishio la wafamasia feki

● *Matumizi holela ya Powercef hatari*



YALIYOMO

Uk-4: Haya ya-jengewe mnara

Uk-5: Samia atamani kuwa Samia

Uk - 7: Mhubiri bangi kura rais?



JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Anza, dumu na Pambazuko

Leo, Jumatatu ya Julai 11, 2022 wewe unakuwa mmoja wa wasomaji wa kwanza wa gazeti la Pambazuko, ambalo litakuwa likikufikia bila gharama yoyote kupitia njia za kisasa za mawasiliano; simu yako ya mkononi na hata kompyuta.

Pambazuko ni gazeti-teke linalochapishwa kwa Kiswahili na kusambazwa kwa njia rahisi ya WhatsApp na mifumo mingine ya mitandao ya kijamii, kwa lengo kubwa la kusambaza habari zilizofanyiwa kazi kwa kuzingatia miiko yote ya kukusanya na kuchakata habari kabla ya kufikia umma; ikiwa ni pamoja na habari za kweli, zenye kuzingatia staha ya binadamu na utu wake.

Ni gazeti lililosajiliwa na Serikali ya Tanzania na kuanza kuhaririwa katika nchi hiyo, lakini kila baada ya muda maalum, litakuwa likihamisha usimamizi kwenda nchi nyingine ambako kuna wahariri wake; Kenya, Uganda na Rwanda,

Gazeti hili, pamoja na kusambaza habari, pia ni uwanja mpana wenye fursa kwa kila mmoja kutoa maoni yake na kuhakikisha kupitia Pambazuko, yanafika kwa taasisi zenye kisimamia nguzo za uamuzi katika nchi; serikali, bunge na mahakama.

Pamoja na kuwa gazeti hili ni chombo cha dunia, kwa imani kwamba kupasha habari hakuna mipaka kwa sasa, lakini walengwa wakubwa wa awali ni watumiaji wa lugha adhimu ya Kiswahili-ikiwa ni pamoja na wanafunzi wa lugha hiyo - wengi wakitoka

Afrika na wengine wakiwa mae-neo mengine nje ya bara hilo.

Katika kuhakikisha Kiswahili kinakuwa na 'kupasua anga,' kurasu moja ya Pambazuko, itabeba darasa la kufunza kwa yeyote anayependa kuelewa lugha hiyo inayokadiriwa kuwa na wazungumzaji wanaozidi milioni 300 duniani.

Msukumo wa kuanza Pambazuko umejengeka katika misingi mingi, mkubwa ukiwa ni kukubalika kwa wazo letu kwa wadau na kushikwa mkono na marafiki wa haki ya kupata habari, Simon Allison, Kiri Rupiah na timu ya gazeti la The Continent. Tunashukuru sana.


Ombi letu kubwa kwako mso-maji wa Pambazuko, ni kusaidia kusambaza gazeti hili kwa marafiki wote, ndugu na jamaa ili kila mmoja apate haki hii na kuwa chanzo cha kukuza maarifa na kutambua kinachoendelea duniani.

Tunaomba kila mmoja awe ba-lozi wa kazi hii iliyotukuka ambayo, pamoja na gharama zake, tumeamua kuibeba na kuifanya bure kwa sasa.

Sisi binadamu, tusifurahie Ukuu wa Mungu pekee kwa kupambazua siku, bali kwa kuanza kusoma Pambazuko kila Jumatatu ili kupata fursa zaidi ya habari.

Karibu sana.

Simon Martha Mkina
Mhariri Mkuu Kiongozi



Jisajili kupata Pambazuko

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa nam-
ba hii ya simu: 0744 768263 kwa kutuma neno
“HABARI” ili kupata Pambazuko kwenye
WhatsApp
- Pia jisajili kwa kutumia Email hii: pam-
bazuko1@protonmail.com ili gazeti la Pamba-
zuko likufikie kupitia email yako, andika neno
“HABARI” nawe utakuwa umejisajili.

Haya yajengewe mnara wa kumbukumbu

Na Plato Hekimachius

KUNA mambo yanatokea mara kwa mara na kujijengea kanuni kuwa ni ya kawaida na yataendelea kutokea. Yamekuwapo katika harakati za kupigania uhuru, yakaendelea baada ya uhuru na yanaendelea hata sasa, zaidi ya nusu karne tangu Tanzania ipate uhuru. Haya mambo yanahitaji kujengewa mnara wa kumbukumbu na yakubaliwe kuwa ni sehemu muhimu ya historia ya ukombozi. Nitajadili matatu kwa ufupi.

Kwanza, ukipenda madaraka, usiogope kifungoni.

Ukiwa nje ya mfumo na unapigania ili uingie madarakani, ni bora kujiandaa kisaikolojia kuwa kifungoni. Aidha, ukiwa madarakani na unapenda hayo madaraka, ujiandae kisaikolojia kuwa ipo siku utajikuta kifungoni ukiwa madarakani au hata baada ya kutoka madarakani.

Uwepo wa kinga za kisheria ndani ya katiba za nchi, hauzuii mtu kuwekwa kifungoni. Hii ni kwa sababu hata wale wasiokuwa madarakani, wana kinga isiyoyandikwa kwenye katiba, lakini walio madarakani huzipuuza na kuwaweka kifungoni. Mnyumbuliko huu ndio hujenga mazoea ya unasaba kati ya kifungo na madaraka. Viongozi wa kisiasa waliofanikiwa katika maisha ya kisiasa ni wale waliokubali kuwa kifungo na madaraka ni ndugu wa damu.

Pili, ukipenda kutetea haki, kubali kudhalilishwa.

Haki ni kinyume cha dhuluma. Kwa hiyo ukitetea haki unaingia katika vita na dhuluma. Mfumo wa dhuluma una watetezi wake pia na wako katika tasnia zote. Kwa hiyo ukiigusa dhuluma, watetezi wake huinuka na kupambana na watetezi



wa haki. Njia maarufu ya kukabiliana na watetezi wa haki ni kuwadhalilisha kwa uwongo, kuwaita majina mabaya, na hata kuwatishia kifo.

Hali hii huwaweka watetezi wa haki wote kuwa tayari kutukanwa na kudhalilishwa wakati wowote. Udhhalilishaji wa watetezi unahitaji kujengewa mnara wa kumbukumbu kwa sababu ni sehemu muhimu isiyobadilika. Watetezi wa haki duniani kote yawapasa kujiandaa kisaikolojia kukabiliana na kuizoea hali hii.

Tatu, ukipenda Habari za uchunguzi, uwe tayari kufungwa.

Habari za uchunguzi katika tasnia ya habari ni kiungo muhimu kinachoongoza heshima ya tasnia hiyo. Lakini, heshima hiyo ina gharama kubwa kwa waandishi. Serikali nyingi pamoja na kujinadi kuwa za kidemokrasia, lakini linapofika suala la habari za uchunguzi, serikali hizo hutumia sheria kandamizi kuzuia habari hizo.

Mbinu zinazotumiwa na serikali hizo ni pamoja na utaratibu wa 'kulesenisha' habari, kufanya usanii wa kukiri uwepo wa sheria kandamizi, lakini bila kuchukua hatua ya kuzifuta, na kutumia wana habari wenyewe kuwa wasimamizi wa mifumo kandamizi ya habari za uchunguzi. Kilele cha dhuluma dhidi ya habari za uchunguzi ni uwepo wa kisinzio cha uchochezi na kuhatarisha usalama wa nchi.

Kwa hiyo, ukiwa mwandishi wa habari za uchunguzi ni vyema kuwa tayari kufungwa, kufungwa, kufilisiwa na kuvurugwa kimapato.

Mnara huu unahitajika kujengwa ili kuthibitisha uwepo wa uhasama wa kudumu katika habari za uchunguzi na serikali zisizopenda uwazi na utawala wa sheria.

Ghana

**Samia
atamani
kuwa Samia**



Rais Samia Suluhu Hassan

BAADA ya Tanzania kupata kiongozi wake wa kwanza mwanamama, Rais Samia Suluhu Hassan, idadi kubwa ya wanawake wanatamani kufika alipo.

Siyo Tanzania tu, au Afrika, bali mashariki ya mbali, Ulaya, Marekani na maeneo mengi duniani.



Samia Yaba Nkurumah

Miongoni mwao ni mto- to wa pili wa rais wa kwan- za wa Ghana huru, Nkwame Nkurumah, aitwaye Samia Yaba Nkurumah (62) ambaye tangu Rais Samia aingie Ikulu,

amekuwa akieleza kufuata nyayo zake kuongoza nchi hiyo.

Samia Nkurumah kwa sasa ni mwenyekiti wa chama alichosisi baba yake, CPP Aliwahi kuwa mbunge wa Jimbo la Jomoro, kabla ya kuamua kuweka nguvu zaidi kuimarisha chama kwa lengo la kuongoza nchi hiyo iliyopata uhuru wake 1957.

Endapo ndoto zake zititimia, Afrika itakuwa na kiongozi mwingine wa nchi anayelitwa Samia.

Sayansi

Ona mara tatu zaidi

TIMU ya wataalamu wa kutibu macho wa Chuo Kikuu cha California, Marekani wamegundua lenzi bandia zinazovaliwaa juu ya mboni, zikiwa na uwezo wa kuona mara tatu zaidi – hata wakati wa mwanga mdogo. Hivyo, sasa watakaovaa lenzi hizo watakuwa na uwezo wa kuona mwezi na nyota kwa ukaribu zaidi.

Afrika Kusini

‘Penda usipende, nitakuwa rais’

KIONGOZI wa chama cha EFF na mmoja wa wabunge machachari wa upinzani nchini Afrika Kusini, Julius Malema ameapa kuwa rais wa nchi hiyo na kwamba wanaomchukia na kumzushia uongo, “wajiandae.”

Pamoja na kwamba hajasema lini ataingia Ikulu na kwa njia gani, lakini amekuwa akirejea kauli hii kwa madai kuwa wananchi wamekichoka chama tawala, ANC ambacho alikuwa kiongozi wake wa vijana kabla ya kuondoka na kuanzisha EFF, chama chenye idadi kubwa ya mashabiki vijana.

Hapa na Pale

6

Libya

Mzimu wa Ghaddafi watafuna Libya

WAKATI wa utawala wa Rais wa Libya, Kanali Mouamar Ghaddafi, hali ya maisha ya wananchi ilikuwa ya kupigwa wafano kwa ubora wake.

Hata hivyo, baada ya kuuawa kwake na wananchi wake wenyewe, wakisaidiwa na Umoja wa Kujihami wa Nchi za Ulaya na Marekani (NATO) nchi zilizotamani



aondoke madarakani kwa kisignizio cha Ghaddafi “kuminya demokrasia nchini mwake.” Aliuawa kwa risasi Oktoba 20, 2011

katika Mji wa Sirte.

Akiwa rais wa nchi hiyo tajiri kwa mafuta, wananchi wake hawakulipa ankara za maji, umeme, elimu bila malipo na wagonjwa walipata matibabu bure. Vijana walihimizwa kuoa na kulipiwa mahari na fedha za fungate na pia gawio la kuanzia maisha.

Wananchi baada ya kulewa maisha ya bure, wakatamani maisha mengine, wakaungana na NATO kumuua Ghaddafi, hata hivyo, sasa wanatamani angerudi. Haiwezekani. Walimuua na wanapambana na maisha magumu kila uchao, huku waliosaidia kumuua kiongozi wao wakika pembeni. Hawana msaada tena.

Sasa maisha yamekuwa magumu, kila uchao wanaandamana na kufanya vurugu, ikiwamo kuchoma majengo ya seri-

kali, bunge na wamejaribu hata kuivamia Ikulu ya Tripori, wakishinikiza kwamba bei ya vyakula ishuke, wapate matibabu bure, walipwe fedha za kujikimu kila mwezi na mzunguko wa fedha uguse mifukoni mwao, mambo ambayo serikali iliyoko madarakani haiwezi, iko “bize” kushughulikia machafuko na minyukano ya wenyewe kwa wenyewe wakigombea madaraka.

Rwanda

Maono ya Kagame

RAIS Paul Kagame wa Rwanda Ramesema anatamani kuona Afrika ikiacha kutegemea wafadhili kupata maendeleo.

Anasema inawezekana Afrika kujitegemea na kuwa na mafanikio makubwa ya uchumi kwani ina mtaji wa watu, rasilimali anuai na watu wenye uwezo wa kufanya kazi, lakini inashindwa kwa kuwa viongozi na watu wengi hawana uthubutu.

Iran

Binti wa rais kortini kwa kufuru

MTOTO wa kike wa rais wa zamani Lwa Iran, Akbar Hashemi Rafsanjani ameshitakiwa kwa madai ya kukufuru utawala wa Jamhuri ya Kiislamu ya Iran kupitia mitandao ya kijamii.

Faezeh Hashemi (59), mbunge wa zamani na mwanaharakati wa haki za wanawake nchini humo, anatumiwa kufanya kufuru hiyo Aprili, mwaka huu.

Serikali ilimfungulia mashtaka mahakamani na kutakiwa kukiri na kuomba msamaha kwa maneno yake kwamba kuondolewa kwa Iran katika orodha ya nchi zinazofadhili ugaidi ni kuharibu ukweli unaofahamika.



Kenya: Uchaguzi Mkuu

Mhubiri bangi, fisi kuongoza Kenya?

Na Mwandishi Wetu

UCHAGUZI Mkuu wa Kenya unaofanyika Agosti 9, mwaka huu – 2022, umejaa pilikapilika na mbwebwe za kila aina kutoka kwa wagombea, wanachama wa vyama vya siasa na mashabiki, huku swali kubwa likiwa – nani atakuwa rais wa moja ya nchi hiyo ya Afrika Mashariki?

Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Kenya (IEBC) imepitisha majina manne ya wagombea urais baada ya kupitia mchakato wa kuchuja wanasisia 57 walioweka nia kuwania ajira namba moja.

Waliopitishwa kuwania ajira hiyo kuu – urais ni Dk. William Samoei Ruto wa muungano wa vyama - Kenya Kwanza, Raila Amollo Odinga kupitia Azimio la Umoja, Prof. George Luchiri Wajackoyah kupitia Roots, huku David Mwaure Waihiga, akiwakilisha Chama cha Agano.

Takwimu zinazotolewa na taasisi za utafiti kuhusu mshindi wa nafasi ya urais na baadhi ya vyombo vya habari zinaonyesha wagombea wawili; Naibu Rais, Ruto na Raila wakipewa nafasi ya mmoja wao kuibuka mshindi kutokana na sababu mbalimbali, kubwa ikiwa ni kuungwa mkono na makabila makubwa ya nchi hiyo; Kikuyu (idadi yao ikikadiriwa kuwa wa milioni 8.14), Waluhya (milioni 6.82), Kalenjini



Mgombea urais wa Kenya kupitia Chama cha Roots, Prof. George Wajackoyah akiwa na mgombea mwenza, Justina Wambui. (Picha: Dennis Onsongo - Nairobi News).

(milioni 6.35), Wajaluo (milioni 5) na Wakamba (milioni 4.6). Ruto ni Mkalenjini. Raila ni Mjaluo. Pia wana ukwasi mkubwa.

Kundi la vijana, wakiwa ndiyo wenye idadi kubwa ya wapiga kura, limeanza kuwatisha wagombea hao wawili baada ya kuonekana likimshabikia gombea asiyepewa uzito mkubwa katika kin-yang'anyiro hicho, Prof. Wajackoyah.

Prof. Wajackoyah alisema akishinda, ataanza kuwalipa mishahara kila baada ya wiki mbili, huku siku za kufanya kazi zikiwa nne; Jumatatu, Jumanne, Jumatano na Alhamisi. Huyu anahubiri “utajirisho kwa njia rahisi.”

Pamoja na kuhubiri kilimo cha bangi, Prof. Wajackoyah anaeleza kutowahi kutumia bangi, mmea unaoelezwa na wataalamu wa afya kuwa chanzo kikubwa cha ma-

gonjwa ya akili kwa watumiaji, ingawa msomi huyo anadai madhara yake kwa afya ni madogo ikilinganishwa na faida kubwa ya uchumi. Kilo 100 za bangi huuzwa hadi Shilingi za Tanzania milioni 60 nchi za Asia.

Prof. Wajackoyah – anayezungumza lugha 11 kwa ufasaha, pia anahimiza ufugaji na hatimaye kuvuna sumu ya nyoka. Anaeleza kwamba sumu ya nyoka ina bei kubwa Ulaya kwani inahitajika kwa ajili ya kutengeneza dawa za kutibu magonjwa ya binadamu. Anadai kwamba lita tano ya sumu ya nyoka aina ya black mamba (koboko) huuzwa hadi shilingi milioni 350 (dola za Marekani 154,000).

Pia profesa huyo anahubiri na kuhimiza Wak-enya kuanza kufuga fisi kwani nyama yake na viungo vingine, ihitajika zaidi nchi za Asia, hasa China.

Zimebaki siku 29 Wakenya kuamua

Mhariri auza tuzo kusaidia watoto Ukraine



Dmitry Muratov, Mhariri wa gazeti la Novaya Gazeta, akiwa na nishani yake ya Nobel (Jason Szenes/EPA-EFE/Shutterstock)

Dmitry Muratov, mshindi mwenza wa Tuzo ya Amani ya Nobel ya 2021 na mhariri wa gazeti la Novaya la Urusi, ameamua kupiga mnada nishani yake kwa Sh. bilioni 240 (dola za Marekani 103.5 milioni) ili kusaidia watoto walioathiriwa kwa vita nchini Ukraine.

Russia iliivamia Ukraine kwa kudondodha komora lake la kwanza Februari 24, mwaka huu.

Mapato yote ya nishani hiyo yataelekezwa kusaidia watoto hao – walio nchini humo na hata waliokimbia, kwa kuwahudumia kwa chakula, dawa na malazi. Taarifa zinaeleza kwamba zaidi ya watoto 250 wamefariki, 446 kujeruhiwa, huku 142 hawajulikani walipo kufuatia kuanza kwa vita hivyo, ambavyo sehemu kubwa ya dunia inailaumu Russia kwa kuvianzisha bila kuwa na sababu zenye mashiko. Hata hivyo, Russia imekuwa ikijibu kwamba ina sababu kubwa ya kupiga Ukraine; “kulinda usalama wake.”

Mhariri huyo ambaye kwa sasa anashii uhamishoni baada ya “kukosana na Rais Vladimir Putin” anakuwa mhariri wa kwanza duniani kutoa msaada mkubwa wa fedha kusaidia watoto wenye madhila kwa wakati mmoja.

Machi, mwaka huu, Rais Putin alimpa onyo kali mhariri huyo kwa madai ya gazeti lake na hata maoni yake, kugegemea upande wa Ukraine katika kuandia habari za vita hivyo. Gazeti hilo baada ya vitisho kadhaa, liliamua kusitisha uchaphishaji, huku Dmitry akisema atarejesha shughuli za gazeti hilo baada ya Russia kusimamisha vipigo kwa Ukraine.

Mnada wa nishani hiyo uliofanyika New York, Marekani Juni 20, ulihudhuriwa na matajiri, viongozi wa taasisi za misaada na uongozi wa juu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (Unicef) na wanunuzi walipatikana kwa njia ya mtandao na wengine kupiga simu. **The Washington Post**



Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com

Mezani kwa Chahali

Katiba mpya, CCM iaminike?

CHAMA tawala nchini Tanzania, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kinaonekana kubadili msimamo wake kuhusu kupatikana katiba mpya inayoendana na mazingira na wakati wa sasa.

Mara kadhaa, viongozi wengi wa chama hicho kilichodumu madarakani kwa zaidi ya miaka 45, wamekuwa wakibeza mchakato wa kupatikana katiba mpya kwa maelezo hafifu kwamba – “tangu lini katiba ikakuletea ugali mezani?”

Hata hivyo, Juni 22, mwaka huu, CCM kupitia kwa katibu wake mwenezi, Shaka Hamdu Shaka imeonyesha nia ya “kubadili gia angani” – baada ya kueleza kuwa Halmashauri Kuu ya chama hicho imeona umuhimu wa kupatikana katiba mpya kwa kuzingatia mazingira ya sasa.

Shaka ilieleza kuwa chama hicho tawala kimeshauri Serikali kuona namna bora ya kufufua, kukwama na kukamilisha mchakato wa katiba mpya kwa maslaha mapana ya taifa na Watanzania wote.

Hata hivyo, habari hiyo haikuonekana kugusa hisia za Watanzania wengi, angalau kwa kutupia jicho mapokeo kwenye mitandao mbalimbali ya kijamii, hususan Twitter ambayo imejikita zaidi kwenye masuala ya siasa.

Wachache walijadili habari hiyo, huku ikibainika kuwa ni baadhi ya makada wa chama cha upinzani Chadema, ambao walionekana kuituhumu CCM kuwa imekuja na taarifa ya uamuzi huo ili kuepesha mjadala unaoendelea kuhusu mgogoro wa ardhini kati ya serikali na Wamasai huko Loliondo na Ngorongoro.

Licha ya mapokeo hayo duni, habari hiyo bado ina uzito mkubwa, kwani huenda ikabadili uepo wa kisiasa nchini Tanzania.

Kwa muda mrefu, ajenda ya umuhimu wa kuwa na katiba mpya imekuwa ya vyama vya upinzani hususan Chadema na baadaye ACT-Wazalendo.

Hata hivyo, vyama hivyo vinatofau-

tiana kuhusu jinsi ya kupata katiba hiyo mpya. Wakati Chadema wanataka katiba mpya ipatikane kwanza kisha ndio unanze mchakato wa kupata Tume Huru ya Uchaguzi, ACT-Wazalendo wanasimamia kwenye kupata Tume Huru ya Uchaguzi kuelekea kupata katiba mpya.

Kwa mtazamo chanya, kuingia kwa CCM kwenye mjadala huo wa katiba mpya kunaweza kuupanua mjadala huo na hivyo kuwezesha ushiriki wa Watanzania wengi zaidi kinyume na hali ilivyo sasa ambapo mjadala huo umekuwa kama ni hakimiliki ya Chadema na ACT-Wazalendo.

Pamoja na CCM kudandia sasa mchakato huo, kwa mtazamo hasi, yayumkinika kuwa chama hicho tawala hakina dhambi ya dhati ya kupatikana kwa katiba mpya, kwa sababu moja kuu: upungufu wa katiba iliyoopo unakinufaisha kwa mizania pana chama hicho tawala.

Bila kujali mitazamo hiyo chanya na hasi kuhusu CCM kujiingiza kwenye mjadala wa katiba mpya, kuna uwezekano mkubwa wa chama hicho tawala “kupora mjadala huo” na kuwaacha Chadema na ACT-Wazalendo wakihangaika wasimamie wapi – Pamoja na kuwa na misimamo yao inayotofautiana.

Ikumbukwe tu kwamba kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, CCM ilifanikiwa “kupora ajenda ya vita dhidi ya ufisadi” na ilikuwa turufu yake muhimu katika ushindi wa mgombea wake wa nafasi ya urais wa Jamhuri ya Muungano, John Pombe Magufuli (sasa marehemu).

Huenda pia, kwa ujanja wa kisiasa - ikatumiya njia zozote kuhakikisha inakuwa kina wa mchakato huo kwa njia ileile inayoweza kulinufaisha chama hicho tawala na kuwaacha wapinzani wake; ama wakiparurana wenyewe kwa wenyewe bila kujua adui yao halisi au kurubuni mmoja wa wapinzani kwa “ushindi” wake.

Tishio la wafamasia feki

Na Waandishi Wetu

BILA shaka, mtu yeyote anayepatikana kodi jeupe ataonekana kuwa daktari au mfamasia aliyehitimu, lakini mtu huyo anayesimama mbele ya makasha na chupa za dawa anaweza kuwa muuaji wako, badala ya kuwa mwokozi anayetarajiwa.

Hali hii ya kuwepo wafamasia wengi wanaouza dawa, inaweza kuonekana neema kwa nchi kwa kuwa na idadi kubwa ya wataalamu hao.

Lakini uchunguzi uliofanywa na Pambazuko, unaonyesha kuwa watu wengi wanaouza dawa na pengine kutoa ushauri wa kitabibu, siyo wataalamu waliosomea taaluma hiyo muhimu.

Pambazuko imebaini kuwa kuna idadi kubwa ya wauza dawa za binadamu wasiokuwa na taaluma hiyo, huku wengine wakiwapa wagonjwa ushauri wa kitabibu kuhusu magonjwa yao.

Pamoja na kutokuwepo takwimu sahihi za idadi ya wauza dawa wasiokuwa na taaluma hiyo, lakini Pambazuko limebaini vijiji vya mikoa wa Tanga na Manyara, vinaweza kuongoza kwani hata maduka ya dawa mengi hayajasajiliwa.

Kutokana na hali hiyo, hivi karibuni, Serikali ya Tanzania, kupitia Baraza la Famasia Tanzania (PC) ilianzisha msako wa nchi nzima dhidi ya maduka ya dawa ambayo hayajasajiliwa na pia kuwa na wakemia wasio na sifa. Jumla ya maduka 23 ya biashara yalifungwa katika Jiji la Dar es Salaam, kitovu cha biashara nchini humo.

Katibu na msajili wa baraza hilo, Elizabeth Shekalaghe aliliambia Pambazuko kuwa msako mkali wa kuwafichua na kuwachukulia hatua za kisheria wamiliki wa maduka ya dawa ambayo hayajasajiliwa ni endelevu na utafanyika nchi nzima.

Takwimu zinaonyesha kuwa Tanzania,

Kenya na Uganda, zinaweza kuwa na maduka ya dawa 7,000 ambapo asilimia 81% yapo vijijini, hivyo wanaojifanya wafamasia, wasiokuwa na sifa - wanaofanya kazi za kitaaluma kinyume cha sheria, wanaweza kuwa wengi zaidi hivyo kuhatarisha maisha ya watu.

Tanzania inatajwa kuwa na wafamasia 3,040 waliosomea taaluma, kusajiliwa na kuthibitishwa na serikali. Kwa kukokotoa, kila mfamasia mmoja anahudumia watu 19,737.

Mbali na changamoto ya kuwa na wafamasia feki, uchunguzi zaidi uliofanywa kwenye viunga vya Dar es Salaam umebaini kwamba maduka mengi ya dawa yasiyokuwa na wataalamu, yamekuwa yakiuza na kutoa maelekezo ya matumizi kwa dawa zinazohitaji utaalamu na uchunguzi mkubwa wa mgonjwa kabla ya kutolewa.

Miongoni mwa dawa inayouzwa zaidi - kwa kutolewa kiholela ni Ceftriaxone - ambayo inajulikana kwa jina la biashara; Powercef.

Uchunguzi wa Pambazuko uliofanywa kwa wiki tatu katika vituo vitatu vya afya na kliniki za kibingwa wilayani Kinondoni, umethibitisha kuwa wagonjwa wengi wanaofika kupata matibabu, asilimia 90 wamekuwa wakitibiwa kwa Powercef, dawa inayoelezwa kutibu magonjwa mengi.

Wagonjwa wengi waliotibiwa kwa dawa hiyo, iliyobatizwa jina la "Sindano ya Mungu" na baadhi ya madaktari, waliozungumza na Pambazuko, wamesema hutibu kwa haraka zaidi magonjwa ya kifua, udhaifu wa mwili na maambukizi katika damu.

Madaktari waliohojiwa walisema Powercef ni miongoni mwa dawa zinazochomwa kwenye mishipa, zenye uwezo mkubwa wa kupambana na magonjwa anuai, ambapo pia hutibu kwa haraka

Tishio la wafamasia feki

homa ya uti wa mgongo, nimonia, maambukizi kwenye njia ya mkojo, magonjwa ya zinaa na maambukizo mengine ya bakteria.

Katika vituo ambavyo waandishi wetu walitembelea, sindano moja ya Powercef inauzwa kwa Sh. 7,000 (Dola za Marekani 2.70).

Dkt. Isaac Maro, mmoja wa matabibu mashuhuri nchini, amekiri matumizi makubwa ya dawa hiyo akitaja sababu mbili za madaktari “kukimbilia” Powercef; uvivu wa baadhi ya madaktari katika kuchunguza sababu halisi za ugonjwa na kujipatia fedha za haraka.

“Kuna ushahidi wa wazi kwamba Powercef inatumika kupita kiasi, na mbaya zaidi hata baadhi ya maduka ya dawa au zahanati, wanaojita madaktari wanaiuza kiholela...”

... Dawa hii ya vijiuasumu (antibiotic) ina nguvu, ni madaktari waliohitimu vyaoni tu ndio wanaoruhusiwa kuwapatia wagonjwa baada ya matokeo ya uchunguzi wa maabara ya kitabibu, siyo vinginevyo,” anaonya.

Dkt. Isaac anaeleza kuwa miongoni mwa madhara makubwa kwa matumizi holela ya dawa, hasa vijiuasumu ni kujenga usugu kwa magonjwa, kuongezeka kwa magonjwa ya ini na pia kupunguza nguvu ya kinga kwa watu.

Naye Mganga Mfawidhi wa zahanati ya Nyota Njema iliyopo Mwenge, Dar es Salaam, Kassim Mwaluko, anasema Powercef ambayo haipendekezwi kutumika kwa watoto wachanga na wanaozaliwa kabla ya wakati kutokana na hofu ya kuongezeka kwa hatari ya madhara, inapaswa kutumiwa kwa uangalifu mkubwa na wahudumu wa afya waliopewa mafunzo.

“Powercef, kama jina linavyoonyesha, ina nguvu na ufanisi katika kutibu baadhi

ya maambukizi, lakini inaweza kuleta madhara ikiwa inatumwa vibaya na mara kwa mara kwa magonjwa; kwa hivyo, haiipaswi kuchukuliwa kama tiba ya kwanza kwa kila ugonjwa,” anaonya.

Dk. Mwaluko anawasihi madaktari wenzake kumtibu mgonjwa kwa Powercef tu baada ya uchunguzi wa kimaabara ili kuepuka kuwa sugu kwa matibabu.

Naibu Waziri wa Afya, Dkt Godwin Mollel akizungumza na Pambazuko anasema kuwa madaktari wanapaswa kuwa makini na dawa ambazo zinahitaji matokeo ya uchunguzi wa kimaabara kabla ya kutumika kwa mgonjwa.

“Mara nyingi serikali imekuwa ikiagiza matumizi makini ya dawa – hasa za vijiuasumu na zisitumike kiholela, hasa zile zenye kuhitaji matokeo ya maabara,” anaeleza Dkt Mollel.

Mganga Mkuu wa Serikali Tanzania, Dkt. Aifello Sichelwe anakiri dawa hiyo imeonekana kutumika zaidi katika kipindi cha miaka miwili iliyopita kutokana na kuwepo matatizo mengi ya mfumo wa upumuaji.

Dkt. Sichwale anasema pia mahitaji makubwa yanaweza kuwa ni matokeo ya ufanisi wa dawa hiyo pamoja na upatikanaji wake nchini, lakini pia anawashauri madaktari kutoitumia kiholela kama tiba ya kwanza kwa kila mgonjwa.

“Nina matumaini sana kwamba madaktari wanajua wakati na jinsi ya kuagiza mgonjwa atibiwe kwa Powercef, lakini lazima wawe waangalifu wasiitumie vibaya ili isiwe sugu kwa sababu ya kutumiwa kupita kiasi,” anaonya.

Hivi karibuni, Shirika la Afya Duniani (WHO) lilitangaza kuibuka kwa kasi kwa matumizi ya dawa za vijiuasumu katika nchi za kitropiki kutokana na kuwepo kwa maambukizi ya Corona na kuonya matumizi holela ya dawa hizo.

China yakengeuka kusaidia Afrika

Na Tryruckia Mfinanga

YAPO mabadiliko makubwa ya mfumo, utendaji na ushiriki wa China katika uhusiano wake na nchi za Afrika, hasa baada ya kifo cha muasisi wa siasa za kikomunisti (ujamaa) na kiongozi wa nchi hiyo ya Bara Asia, Mao Tze-Tung.

Tangu awali, Mwenyekiti Mao, kama alivyozoeleka kuitwa, alijenga misingi ya kusaidia Afrika – kwanza nchi zake ziji-tawale kutoka kwenye makucha ya kutawaliwa na baada ya uhuru, alifanya kila aliloweza kuhakikisha maendeleo ya nchi huru yanaonekana na kugusa wananchi, wengi wakiogolea kwenye ufukara.

Baada ya uhuru wa nchi za Afrika, China ilianza ushirikiano na nchi hizo na kujikita kusaidia ujenzi wa miundombinu yenye tija kiuchumi – ikipiga vita umasikini; ujenzi wa mifumo ya kupiga vita magonjwa – ikijenga hospitali na kuleta madaktari bingwa pamoja na misaada ya dawa; ujenzi wa miundombinu ya kukuza elimu – ikijenga shule na vyuo au kupokea Waafrika kwenda kusoma China.

Hata hivyo, baada ya kifo cha Mwenyekiti Mao, China aliyoiacha kiongozi huyo ilibadilika na kushindwa kuitofautisha kwa kiasi kikubwa na nchi zingine ambazo zilitajwa kuwa za mabeberu.

Katika miaka ya hivi karibuni, China imegeuka kuwa kinara wa kutoa mikopo yenye riba kubwa kwa Afrika. Inadaiwa kuwa hivi sasa China inadai riba ya hadi asilimia 5.07, tofauti na awali ambapo riba ilikuwa haizidi asilimia 3, huku miko-pi ikiwa ya muda mrefu.

Pamoja na kupunguza kwa kiasi kikubwa misaada kwa Afrika, China inaonekana kuweka pembeni utaratibu aliyoucha Mwenyekiti Mao wa ujenzi wa miundombinu kwa nchi masikini na sasa imegeuka mbinu za kufurahisha watoa uamuzi; viongozi wakuu wa serikali na wabunge. Mbinu zilizozeleka kutumiwa na nchi nyingi za mabeberu katika



Mao Tze-Tung.

kushawishi fursa za biashara na uwekeza-ji wenyewe sura za kinyonyaji.

Mbinu hizo ni kujenga majengo ya kiasa ya makazi ya viongozi wa nchi, ikulu, vituo vya mikutano na mabunge - lengo kuu likiwa kugusa moja kwa moja mawazo ya watoa uamuzi ili “kuwalainisha” panapotokea fursa zenye manufaa ili China ipate wepesi.

Vyanzo mbalimbali vinaeleza kuwa China – kwa miaka 30 iliyopita, imejenga ikulu au makazi ya viongozi wakuu wa nchi 24 katika Afrika, huku ikijenga majengo ya bunge na mikutano yanayofikia 162.

Kwa kutaja majengo machache na kiasi kinachoelezwa na China kimetumika kukamilisha majengo hayo ni pamoja na Bunge la Zimbabwe lililojengwa kwa Shilingi za Tanzania bilioni 370, kiasi ambacho kingeweza kujenga barabara ya lami yenye urefu wa kilomita 350 – sawa na umbali wa kutoka Dar es Salaam hadi Tanga.

Kutokana na kukengeuka kwa China, je, bado Afrika iendeele kuona kuwa nchi hiyo tajiri ni rafiki wa kweli na kwamba bado inabeba maono ya Mwenyekiti Mao katika kujenga usawa na ustawi wa Afrika?

Atamani Zanzibar yenye neema



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Othman Masoud Othman (Picha:BBC)

Na Jabir Idrissa, Unguja

SERIKALI ya Umoja wa Kitaifa (SUK) anayoitamani mtaalamu mboenzi wa sheria, Othman Masoud Othman ni ile inayoelekeza kujengea nchi mazingira bora ya siasa, uongozi shirikishi na maendeleo endelevu kwa watu wa Zanzibar.

Anatamani kuona matunda ya nchi yanawafikia wananchi wote bila ubaguzi wa rangi, maeneo wanakotoa ama kuishi na bila kujali ushabiki ama ufuasi wa vya-ama vya siasa.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, anaeleza kuwa kinyume cha misingi hiyo na kushindwa kutekelezwa kwa ahadi za kuimarisha SUK, ni serikali kujichimbia kaburi ambalo linaweza kufukia hata wale wanaohusika kukandamiza na kuminya ustawi wa jamii ya watu wa Zanzibar.

Anaeleza kwamba kukua kwa mgawanyiko katika jamii kunachagiza chuki miongoni mwa wananchi na kusababisha machungu makubwa ikiwamo uonevu wa dhahiri kwa wenye mawazo kinzani na watawala wenye dola.

Moja ya misingi ya kuhakikisha Zanzibar inakuwa na amani muda wote, ni kuwepo kwa Tume Huru ya Uchaguzi ambayo itakuwa msimamizi wa haki wa mchakato mzima wa kufanyika kwa uchaguzi huru, haki na wenye kuleta viongozi walioshinda kihalali kupitia sanduku la

kura.

Mwanasheia Othman aliyewahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Zanzibar, anaeleza kuwa tume iliyopo imekuwa kiini cha matatizo yanayokwamisha maendeleo kiuchumi na kuminya matakwa ya wananchi katika uongozi wa nchi yao.

Othman alieleza hayo hivi karibuni alipokutana na Balozi Mdogo wa Uingereza nchini Tanzania, Rick Shearn aliyemtembelea ofisini kwake Migombani, mjini Zanzibar kwa mazungumzo maalum.

Balozi Shearn alieleza matumaini ya nchi yake kusaidia Zanzibar kutekeleza sera za kupambana dawa za kulevya, kuendeleza hifadhi ya mazingira na kukabili athari za mabadiliko ya tabianchi, maridhiano, umoja wa kitaifa na ujenzi wa mifumo bora ya kuchochea mageuzi ya kisiasa.

Maoni ya Othman yanakuja kipindi ambacho fikra za watu wengi zinahimiza kuwepo utashi wa kisiasa, hasa kutoka chama tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika kushirikiana na vyama vingine, kuchochea mshikamo wa Wanzibari na kuhimiza maendeleo ya pamoja.

Kuna kila dalili kwamba CCM inapendelea zaidi kuona serikali inayoundwa na chama hicho pekee, bila kujali dhamana ya kura – kwa asilimia kubwa kutoka chama kingine na kupuuza misingi ya SUK.

Tutakumbuka Daima...



KWAMBA Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Januari 22, 1962 aliamua kuachia nafasi ya Waziri Mkuu wa Tanganyika na kuchukuliwa na Rashid Mfaume Kawawa (kulia). Hapa ni Ikulu ya Dar es Salaam baada ya Mwalimu kutangaza uamuzi wa kujiuzulu ili kwenda kuimarisha Chama cha TANU. Baadaye Mwalimu alikuwa Rais wa Tanganyika. Mwalimu, kama ilivyo kwa Kawawa, wote ni marehemu. (Picha: Kutoka Maktaba ya Pambazuko).

Jifunze Kiswahili



Na Dkt. Michael Mashauri

KISWAHILI ni miongoni mwa lugha zinazokua kwa kasi kubwa kila siku, siyo Bara la Afrika pekee, bali maeneo mengi. Vyuu vikuu nje ya Afrika, vimeanza kufunza lugha hiyo adhimu. Kutokana na umuhimu wake, Pambazuko limeamua – kila wiki, kuwa njia ya kufundisha Kiswahili bure kwa yeyote anayependa.

Leo darasa linaanza kwa kufunza Sauti na Utamkaji (Sounds and pronunciation)

Irabu (vowels)

Kiswahili kina irabu 5 (Kiswahili has 5 vowels):

a	as in father:	mama (mother)
e	- - ten	: wewe (you -sg)
i	- - see	: mimi (I)
o	- - pot	: nono (fatty)
u	- - put	: kuku (chicken)

Maneno mengine yana mfuatano wa irabu (Some words have vowel sequences)

aa	:	saa (watch)
ee	:	mzee (elder)
ii	:	miiko (taboo)
oo	:	choo (toilet)
uu	:	sikukuu (holiday)

Konsonanti (consonants)

Kiswahili kina konsonanti 25 (Kiswahili has 25 consonants):

b	as in baby :	bibi (grandmother)
ch	- - chair	: chai (tea)
d	- - dady :	dada (sister)
dh	- - that:	adhibu (punish)

f	- -	fat:	fedha (money)
g	- -	got:	gaidi (terrorist)
gh	-	:	ghali (expensive)
h	- - hat	:	hofu (fear)
j	- -	jag	:jicho (eye)
k	- -	cake	:kaka (brother)
l	- -	leg	:lala (sleep)
m	- -	man	:mama (mother)
n	- -	name	:neni (word)
ny	- -	tenure	:nyama (meat)
ng'	- -	sing	:ng'oa (uproot)
p	- -	pit	:pika (cook)
r	- -	race	:ruka (jump)
s	- -	say	:sema (say)
sh	- -	shame	:shati (shirt)
t	- -	ten	:tupa (throw)
th	- -	thing	:thamani (value)
v	- -	van	:vaa (dress)
w	- -	will	:wewe (you-sg)
y	- -	yes	:yai (egg)
z	- -	zoo	:zaa (bear)

m/n can combine with other consonants to make one sound:

mb	as in member	:shamba (farm)
mp	- - hamper	:kampuni(compa-ny)
mw	-	:mwalimu (teacher)
nd	as in sender like)	: p e n d a (l o v e /
nch	- - puncture	:pancha (puncture)
ng	- - language	:nguo (clothes)
nz	- - stanza	:funza (train/teach)
nw	-	:anwani (address)

• *Mwandishi wa Darasa la Kiswahili ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

Tupo njia sahihi uchumi wa gesi



Mitambo ya kusafirisha gesi. (Picha: tovuti ya BBC)

Na David Kafulila, Simiyu

UWEKEZAJI wa Shilingi za Tanzania trilioni 70 unatarajiwa kuongeza chachu ya uchumi imara, endapo mikataba iliyosainiwa na serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan na kampuni tano za biashara ya gesi, itazingatia ustawi na maslahi mapana ya nchi.

Juni 11, mwaka huu, Rais Samia alishuhudia makubaliano ya awali ya uwekezaji wa kiasi hicho kikubwa cha fedha (dola za Marekani bilioni 30), kati ya serikali na kampuni kubwa tano za kimataifa; Equinor, Shell, ExxonMobil, Medco Energy na Pavilion.

Uwekezaji wa Sh. trilioni 70 ni karibu nusu ya uchumi wa Tanzania kwa sasa (Trilioni 41.48).

Huu ni mradi mkubwa unaohusisha weledi katika maeneo mengi ya nishati, biashara na uchumi wa kitaifa na kimataifa, sheria za kitaifa na kimataifa, mazingira na taaluma nyingi zinazohitaji uzoeifu mkubwa.

Ni kutokana na mazingira hayo, kabla ya kufikia makubaliano na kampuni hizo, serikali iliona busara kuwa na wataalamu wabobezi katika mikataba ya mafuta na gesi ili kuepuka “kuingizwa mkenge” na wawekezaji- ambao lengo lao kubwa ni kupata faida nono kila inapowezekana.

Pamoja na kuwepo wataalamu wa ndani, serikali iliingia kandarasi na mshauri mwelekezi; kampuni ya Boots Barker kutoka Uingereza, ili kuangalia kila mwanya wenye uwezekano wa nchi kupata kisichostahili.

Ni kweli nchi yetu ina wasomi na vyo vingi, lakini ni ukweli usiopingika kuwa hatuna hazina yenye uzoeifu wa kutosha kwenda kwenye mezani ya makubaliano mahsusi – hasa kwenye sekta ya mafuta na gesi na kampuni zenye miaka mingi kwenye biashara hiyo.

Baada ya mshauri huyo mwelekezi kupatikana, mitandao ya jamii, iliibuka na mijadala, wachangiaji wengi waki-onekana kupinga hatua hiyo ya serikali kuingia kandarasi na mshauri huyo kutoka nje - wengi wakihoji; je, Tanzania hakuna wenye uwezo wa kushauri?”

Kwenye dunia ambayo nishati ni mwamuzi wa uchumi imara, makubaliano ya serikali na kampuni zinazowezeza, yanachagizwa na misukumo mingi, ikiwemo ujasusi, kwani mafanikio ya nchi kuingia soko la gesi, yanabeba tafsiri kwa nchi washindani zenye sura tofauti kwa kampuni zinazoshindana au nchi. Ndiyo maana, mbinu kama ugaidi huweza kuwa sehemu ya mkakati kukabiliiana.

Ni katika msingi huo, uwekezaji mkubwa kama wa gesi na mafuta, unachukuliwa hadhari nyingi, ikiwamo za kiuchumi na kuisalama kabla ya kufikia muafaka. Mfano, kinachoendelea kutokea Msumbiji baada ya kuonekana nchi hiyo inaweza kuingia mapema kwenye soko la gesi asilia, kwa kuwa na bei nafuu, ugaidi ukapamba mota.

•Kafulila ni Mkuu wa Mkoa wa Simiyu. Makala haya yamehaririwa kwa kuzingatia nafasi ya kurasa na muda wa msomaji.

Mpemba: Mtanzania kijana aliyetikisa dunia ya utafiti

Na Mwandishi Wetu

HAKUNA aliyeamini kuwa maji, au kimiminika chochote, kilichochemka, kikiwa na nyuzi joto kubwa zaidi ni rahisi kuganda kuliko chenye ubaridi, lakini huo ndiyo ukweli ulioiweka Tanzania katika ramani ya wagunduzi mahiri waliowahi kutokea duniani.

Ukweli huo uliwashangaza wanazuoni na wenye elimu kubwa ya sayansi duniani, huku wakishindwa kuamini dhana hiyo ya kisayansi hadi uchunguzi ulipothibitisha. Kuthibitika huku, kuliweka dhana za wanasayansi wenye heshima kubwa na wanaofanyiwa rejea nyingi, kwenye shaka.

Aliyegundua hivyo ni Mtanzania, wakati huo akiwa kijana wa shule ya sekondari, ingawa Tanzania haikuwahi “kutumia nguvu” kumtangaza wala kumpa heshima aliyo-stahili.

Ni ugunduzi wa kisayansi wa Mtanzania usiotajwa sana kwenye vitabu vya shule nchini Tanzania, lakini ni gumzo la kitaaluma katika vyuo na taasisi mbalimbali za elimu za mataifa mengine.

Ugunduzi huu wa kisayansi unaoelezea “sifa ya kipekee ya vimiminika” ulifanywa na mwanafunzi wa kidato cha tatu wa Kitanzania katika Shule ya Sekondari Magamba, Lushoto, Mkoani Tanga, mwaka 1963. Jina la Mwanafunzi huyo ni Erasto Bartholomeo Mpemba, jina ambalo sifa hiyo ya vimiminika imepewa ni “Mpemba Effect.”

Erasto Mpemba, kama ilivyokuwa kwa wanasayansi wengine maarufu duniani, alifanikiwa kugundua sifa hii muhimu

ya maji kama ajali, kama ilivyokuwa kwa wagunduzi wengine wa kisayansi, mfano Friedrich August Kekule (mgunduzi wa udhani wa umbo la kekule katika Sayansi ya Kemia), Isaac Newton, Archemedes na wengine.

Mpemba naye alifanya ugunduzi wake baada ya tukio la kawaida tu katika maisha yake ambalo lilileta majibu yasiyo ya kawaida na yanayofikirisha.

Katika andiko mashuhuri juu ya “Mpemba Effect” lililochapishwa katika Jarida la Kitaaluma la Journal of Physics Education’ la mwaka 1969, Mpemba anaeleza ifuatavyo; “jina langu ni Erasto Mpemba, nitawaambia ugunduzi wangu ambao umetokana na matumizi mabaya ya jokofu”.

Masimulizi hayo ya Mpemba katika andiko hilo yanaainisha kwa undani mazingira ya elimu ya Tanzania tangu miaka ya mwanzo ya uhuru wa Tanganyika na hata sasa kwa baadhi ya maeneo. Kawaida wanafunzi wengi wanaosoma shule za umma, ama hufanya biashara za walimu wakiwa madarasani wakati wa vipindi au baada ya vipindi, au hufanya biashara za wazazi wao.

Erasto Mpemba na wenzake kadhaa katika Shule ya Magamba (hivi sasa ni Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa, Sekomu), walikuwa wanauza ‘ice-cream (barafu)’ baada ya kumaliza vipindi vya masomo.

Ingawa haijawekwa wazi kwenye simulizi hiyo kwamba, mradi huu ulikuwa wa shule ama wa mwalimu, lakini wanafunzi waliohusika na biashara hii walikuwa

Endelea Uk. 18



Mtanzania aliyetikisa

Inatoka Uk. 17


wengi, hivyo iliwabidi wagombe nafasi kwenye jokofu moja wakati wa kutengeneza 'ice cream' hizo. Inaelezwa kuwa wanafunzi walikuwa wakinunua maziwa asubuhi kutoka vijiji vya jirani; Maina, Mazinde Juu, Mabughai na Kost, baadaye kuyachemsha na kuyaacha yapoe kabla ya kuyaweka kwenye jokofu ndipo wanaenda darasani.

Wakimaliza vipindi, huchukuwa 'ice-cream' zilizoganda na kupeleka Lushoto mjini kwa mauzo. Yule atakayekosa nafasi ya kuweka 'ice cream' zake kwenye jokofu, ilimpasa asubiri mpaka wenzake watoe zao nyakati za mchana kwenda kwenye mauzo ndipo na yeye apate nafasi ya kuweka za wakwe.

Lakini pia kwa yule aliyeweka mwanzo kabla ya mwenzake, alikuwa na uhakika wa kuanza kupeleka 'ice-cream' zake sokoni kabla ya mwezake, maana anayeweka mwanzo, zitaganda mapema zaidi kabla ya wengine. Hivyo kulikuwa na changamoto mbili muhimu kwa Mpemba na wenzake, kupata nafasi ya kuweka 'ice cream' kwenye jokofu.

Siku moja wakati Mpemba anachemsha maziwa ya ice-cream, mwenzake aliamua asichemshe maziwa ili awahi nafasi anayoipenda kwenye jokofu kabla Mpemba hajaweka kwenye nafasi hiyo. Kwa akili zake za kitoto, hakujali afya za walaji, bali muhimu kwake ilikuwa kuwahi nafasi ndani ya jokofu. Mpemba aliendelea kuchemsha maziwa, lakini kwa bahati ikawa imebaki nafasi moja tu kwenye jokofu, hivyo naye kwa hofu ya kupoteza hiyo nafasi moja iliyobaki, akaamua kuyaweka yakiwa bado ya moto. Japo alijua ni matumizi mabaya ya jokofu, lakini aliamua kufanya hivyo.

Baada ya saa moja na nusu hivi, wakiwa kwenye mapumziko ya vipindi ya darasani, Mpemba na wenzake walienda kwenye jokofu kuangalia hali ya bidhaa zao na pia usalama wa jokofu. Zaidi Mpemba alikuwa na wasiwasi kwa vile



Newton, utafiti wake ulitikiswa na Mpemba (Picha:Wikipedia)

aliweka maziwa ya moto, hivyo alitaka kwenda kuhakiki usalama wa jokofu.

Alichokiona Mpemba, ndiyo leo dunia inakitambua kwa jina la "Mpemba Effect." Maziwa aliyoweka Mpemba yakiwa ya moto, yaliwahi kuganda kuliko ya mwenzake.

Hali hii ilileta rabsha kwa Mpemba na wenzake, ambao waliamini mwenzao amefanya ujanja wa kubadilisha bidhaa zao na kuwa zake. Hawakuamini kilichotokea. Mpemba naye hakuamini kilichotokea na ugomvi wao ulikuwa mkubwa hadi kufika kwa walimu.

Siku kadhaa baada ya tukio hilo, Mpemba akiwa darasani aliamua kumuuliza mwalimu wake wa kidato cha tatu wa somo la Fizikia juu ya alichokishuhudia, lakini majibu ya mwalimu huyu yalimfanya abadili mawazo kwa muda. Kiufupi, majibu ya mwalimu huyo yalikuwa sawa na ya yule rafiki yake Mpemba kuwa "Mpemba, alichanganya sahani za kuhifadhi ice-cream, hilo jambo haliwezi kutokea."

Baada ya kumaliza kidato cha nne shuleni Magamba, Mpemba alijiunga na kidato cha tano katika Shule ya Sekondari Mkwawa, Iringa (sasa ni tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, MUCE), akichukua masomo ya sayansi. Siku moja wakiwa katika somo la Fizikia wanasoma mada ya joto (heat) wakati mwalimu anaelezea Kanuni ya Newton ya Upojaji (cooling),

Itaendeela wiki ijayo...

Ubingwa Yanga ni mikakati



Wachezaji na viongozi wa Timu ya Yanga wakifurahi kwa kuwa mabingwa wa soka Tanzania; 2022 - 2023. (Picha na Michuzi Blog).

Na Daniel Mbega, Mkuranga

BAO la kichwa la Dennis Nkane dakika ya 81 katika mechi ya mwisho ya kufunga msimu wa Ligi Kuu ya NBC 2021/2022, liliwezesha Timu ya Yanga kumaliza msimu bila kupoteza mechi, ikiwa ni rekodi yake mpya baada ya miaka kadhaa.

Nkane alifunga bao hilo katika mechi dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Tanzania akiunganisha krosi ya Tehiko Ushindi Wakubanza na kuhitimisha rekodi ya ushindi bila kupoteza mechi.

Huo ulikuwa ushindi wake wa 22 katika mechi 30 za msimu huu, huku ikiwa imetoka sare mara nane, ikifunga mabao 49 na kuruhusu mabao nane tu.

Kutokana na kuwa na malengo ya ubingwa, wachezaji wa Yanga walijikuta wakipambana kufa na kupona kupata pointi na kutangaza ubingwa mapema, hata hivyo, sare zilizojitokeza zikawa kikwazo kwao, hivyo kujikuta wakiweka dhamira ya kuhakikisha hawapotezi mechi, kwani kufanya hivyo kungezima ndoto zao za ubingwa.

Ni kutokana na jitihada hizo, hatimaye Yanga ikajikuta iko nafasi ya kupambana kuhakikisha inaweka rekodi ya kutofungwa, ambayo imefikwa huku ikiruhusu mabao machache. Pia kudhihirisha kwamba ngome yake ilikuwa imara kuliko timu zote, kwani Simba iliruhusu mabao 14 na kufunga mabao 41.

Kimsingi, Yanga ilijipanga kutwaa ub-

ingwa baada ya kuukosa kwa misimu minne mfululizo, misimu ambayo ilitawaliwa na mtani wake wa jadi, Simba.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Yanga, Hassan Bumbuli, anasema katika mikakati wa ubingwa wa Yanga, mbali ya kudai kusajili kikosi imara, kocha mkuu wa timu hiyo Mohammed Nasiredine 'Nabby' aliugawa msimu huo katika makundi sita yenye mechi tano kila moja.

Bumbuli anasema, walijiweka malengo ya kuhakikisha kila kundi la mechi zao lazima wakusanye pointi zisizopungua 12 na ikiwezekana wachukue zote 15.

Katika kundi la kwanza la mechi hizo, Yanga ilifanikiwa kutwaa pointi zote 15, Kwenye kundi la pili, timu hiyo ilikusanya pointi 11. Jitihada hizo ziliendelea kwenye kundi la tatu kwa kushinda mechi nne na kutoka suluhu moja.

Kwenye kundi la nne, ambalo ni duru la pili la ligi, Yanga ilishinda mechi nne na kutoka suluhu moja. Huku kwenye kundi la tano ilishinda mechi mbili na moja nyumbani na nyingine kutoka suluhu.

Yanga ilibidi kusubiri mpaka kwenye kundi lake la sita la mechi ili kutangaza ubingwa ambapo iliibuka kwa ushindi katika menchi

Nne na kutoka suluhu moja.

Kutokana na mtiririko huo, ni dhahiri Yanga ilijipanga kushinda ndani ya uwanja na haikuwa bahati wala mipango inayofanywa nje ya uwanja, ikiwamo hongo kwa wachezaji wa timu pinzani kama wanavyodai mashabiki wa watani wao wa jadi.

PICHA KUBWA

PAMBAZUKO ni kama uyoga – kwa kuota popote; ni gazeti litakalomea penye kumea heri na neema; hivyo kupongeza, lakini pia halitaona haya kuota penye wizi, rushwa, uonevu kwa lengo la kung'amua yanayoendelea ili kuhabarisha umma na kutoa nafasi kwa 'watoa uamuzi' kukomesha ushetani katika jamii zetu. Picha hii ilipigwa kwenye shamba la miti, Njombe. (Picha na Simon Mkina)



GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi na Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO).

